17/Agasti/2025



# Mbarawa ataja faida ujenzi SGR Tanzania, Burundi

Na Shakila Mtambo

WAZIRI wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa amezitaja faida za ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa ya SGR ikiwemo kupunguza gharama za usafirishaji mizigo kutoka Tanzania kwenda Burundi.

Profesa Mbarawa alieleza hayo wakati wa hafla ya uzinduzi wa ujenzi wa reli ya SGR kipande cha saba kutoa Uvinza Tanzania hadi Musongati, Burundi jana.

Hafla hiyo iliwakutanisha viongozi kutoka Tanzania na wengine kutoka Burundi akiwemo Waziri wa Fedha, Dk Mwigulu Nchemba.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutawezesha kupunguza gharama za usafirishaji kutoka Dola za Marekeani 3,800 (Sh milioni 9.9) hadi Dola 2,000 (Sh milioni 5.2) kwa kasha moja.

Pia, reli hiyo itawezesha usafirishaji wa mizigo mingi kwa wakati mmoja ikilinganishwa na ilivyo sasa.

Alisema kwa sasa lori moja lina uwezo wa kusafirisha tani 30 lakini reli hiyo ikianza usafirishaji itasafirisha tani 3,800 kwa safari moja.



Reli hiyo pia itatumia nishati ya umeme utakaozalishwa kwa kutumia vyanzo vya asili na kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa ambayo ni ajenda ya nchi nyingi duniani.

Kadhalika reli hiyo itawezesha migodi ya nikeli iliyopo Musongati, Burundi kusafirisha madini yake hadi Bandari ya Dar es Salaam na utaboresha maisha ya watu.

"Itaboresha maisha na uchumi wa wananchi kwa kupunguza gharama za usafirishaji wa bidhaa kutoka Tanzania na Burundi… kwa sasa gharama ya usafirishaji wa kasha moja la futi 20 ni Dola za Marekani 3,800 na reli hii ikikamilika gharama itakuwa Dola 2,000."

Alisema mradi huo utakapokamilika utatoa fursa kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kufanya biashara na kuimarisha utangamano wa kikanda na kuleta ustawi wa jamii.

Aidha, alisema reli hiyo itakuwa na urefu wa kilometa 300 na mradi unatekelezwa na mkandarasi kwa ubia wa kampuni ya China Railway Engineering Group Company Limited (CREC) na China Railway Design and Consultant Group kwa miaka sita (miaka mitano ya ujenzi na mmoja wa matazamio) na gharama yake ni Dola za Marekani bilioni 2.1

Mhandisi Mkuu wa Usafirishaji kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Mumina Wa-Kyendo akimuwakilisha Mkurugenzi Mkaazi wa benki hiyo alisema AfDB itaendelea kutoa ufadhili wa miradi yenye tija kwa jamii kwa lengo la kuboresha miundombinu na ustawi wa wananchi.

CamScanner
CamScanner

Mwananchi Jumapili Agasti 17 Pg2

# Ujenzi SGR Uvinza –Musongati kilometa 240 waiva

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ameshiriki uwekaji jiwe la msingi la ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Uvinza hadi Musongati, akiwahakikishia Watanzania na Warundi kwamba, ujenzi huo utaanza katika muda uliopangwa.

Majaliwa alishiriki hafla hiyo iliyofanyika eneo la Musongati, nchini Burundi jana akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema reli hiyo yenye urefu wa kilomita 240 ikikamilika itakuwa ya kwanza inayounganisha nchi na nchi katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Majaliwa amesema kukamilika kwa ujenzi wa reli kuunganisha masoko na kuendeleza biashara baina ya Tanzania na Burundi.

"Reli ikikamilika itafungua fursa kwa wananchi ambao wataweza kutoka hapa hadi Dar es Salaam ndani ya siku moja. Hata kwenye usafirishaji wa mizigo, hivi sasa lori linatumia saa 96 kutoka Dar hadi Bujumbura lakini baada ya kukamilisha ujenzi, usafirishaji wa mizigo kwa kutumia treni utatumia saa 20 tu," alisema Majaliwa kama alivyonukuliwa katika taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

"Mradi wa reli ya kisasa siyo tu kwamba utarahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo, bali pia utafungua milango ya fursa mpya za uwekezaji na biashara kati ya Tanzania na Burundi," alisema.

Alisema ujenzi wa reli hiyo utagharimu Dola bilioni 2.154 za Marekani na unatarajiwa kukamilika ndani ya miaka mitano. Mwaka mmoja baada ya ujenzi ameeleza utakuwa wa matazamio.

Rais wa Burundi, Evarist Ndayishimiye alisema kuanza kwa ujenzi wa reli hiyo kutatibu shauku ya muda mrefu ya nchi hiyo kuwa na usafiri wa reli.

"Leo ni siku ya furaha kwetu. Tumepata jawabu la tangu enzi na enzi. Mwaka 1921, mradi huu ulianzishwa na Wabelgiji kisha wakaja Wajerumani lakini wakashindwa. Leo hii Tanzania na Burundi tumeweza," alisema.

Alisema Burundi imebarikiwa kuwa na madini mengi na kuna wakati aliitisha kikao cha wawekezaji kutoka nchi kadhaa, wengi wakavutiwa na wakataka kuwekeza mara moja, lakini wakamuuliza wakianza kuchimba madini ya nikeli watayasafirishaje.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Rais wa Burundi, Meja Jenerali Evarist Ndayishimiye (kulia) wakivuta kamba kuashiria ufunguzi wa uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Uvinza hadi Musongati, Burundi jana. **Picha OWM**

"Hiyo changamoto ilitufanya tubungue bongo zetu na kutafuta suluhisho. Tunaishukuru Serikali ya Tanzania kwa kukubali kuungana nasi ili tuanze mradi huu muhimu. Tukitoka hapa, tunataka reli iunganishe hadi Kindu, Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na baada ya hapo, tunataka reli yetu ifike Afrika Magharibi kwenye ufukwe wa bahari ya Atlantiki kwani tunaamini njia hiyo itaharakisha kuleta maendeleo," alisema.

Alimpongeza Rais Samia kwa kufikia hatua kubwa za maendeleo akisema:

"Nimekaa Tanzania kwa muda mrefu lakini kwa sasa nikija naweza kupotea. Magomeni napajua, Tabata na Vingunguti napajua, Mwenge napajua na Kinondoni nilishakaa; lakini kwa sababu ya maendeleo yaliyopatikana, naweza kupotea. Tunamshukuru kwa uongozi wake imara."

Kauli hiyo aliizungumza kwa Kiswahili na kuamsha shangwe miongoni mwa wananchi waliohudhuria tukio hilo.

Awali, Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa alieleza utekelezaji wa mradi huo unakwenda sambamba na Ajenda 63 ya Umoja wa Afrika ambayo inataka Bara la Afrika liunganishwe kwa mtandao wa reli ya kisasa.

Alisema mbali na kuziunganisha nchi hizo mbili, kukamilika kwa ujenzi wa reli hiyo kutarahisisha kupunguza gharama za usafirishaji wa mizigo.

"Hivi sasa, kontena moja la futi 20 linasafirishwa kwa gharama ya Dola 3,800 lakini reli ikikamilika, gharama itashuka hadi Dola 2,000," alisema.

Alisema faida nyingine itakayopatikana baada ya mradi huo kukamilika ni kuwezesha kusafirisha mizigo mingi kwa wakati mmoja. "Hivi sasa, mzigo unaosafirishwa kwa lori moja ni tani 30, lakini reli ikianza kazi, tutaweza kusafirisha tani 3,000 kwa wakati mmoja," alisema.

CamScanner

Jumapili Habari Leo Agosti 17/2025 Pg1






Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye wakipongezana baada ya uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kipande cha saba na nane kutoka Uvinza, Tanzania hadi Musongati nchini Burundi jana. Picha ndogo ni Majaliwa na Rais Ndayishimiye wakiweka jiwe la msingi la ujenzi huo jana. Waziri Mkuu amemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika uzinduzi huo. (Picha zote na Ofisi ya Waziri Mkuu).

CS CamScanner
CS CamScanner

# KIOO CHA JACQUELINE LIANA

**Matumaini>> Mabasi ya mwendokasi yakiongezwa yatamaliza kero ya abiria kukaa muda mrefu vituoni**

## Maswali ni mengi mabasi mwendokasi kuchungulia kaburi-4

JANUARI 11, mwaka jana, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), ulipata mtendaji mkuu mpya, Dk. Athuman Kihamia, kufuatia uteuzi wa Dk. Edwin Mhede kutenguliwa. Kama ilivyokuwa kwa Dk. Mhede ndivyo hivyo kwa Dk. Kihamia, ameingia kuongoza wakala huo wakati kampuni ya mabasi yaendayo haraka (UDART) ikiwa dhoofu hali.

Hata wakati Dk. Mhede alipoteuliwa kuwa mtendaji mkuu wa DART, tayari hali ya mradi huo uliozinduliwa Mei 2016, ulikuwa 'hali si hali'. UDART ni kampuni binafsi inayoendesha mabasi ya yaendayo haraka maarufu mwendokasi, kirefu chake ni Usafiri Dar es Salaam Rapid Transit.

Mabasi yaendayo haraka ni mradi wa kwanza kutekelezwa Afrika Mashariki na wa tatu barani Afrika, ambao kwa awamu ya kwanza umehusisha ujenzi wa kilomita 20.9 za barabara za Kimara – Kivukoni, Faya– Kariakoo na Magomeni – Morocco, vituo vya mabasi 27, madaraja ya waenda kwa miguu matatu na vituo vikuu vitatu.

Utekelezaji wa mradi umegharimu sh. bilioni 403.5 ambapo kati yake sh. bilioni 86.5 zimetolewa na serikali na sh. bilioni 317 ni mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Wakati wa uzinduzi wa usafiri huo, ilielezwa mradi ulikuwa na mabasi 140 na kuahidiwa kuongezeka hatua kwa hatua hadi kufikia 305 kwa awamu hiyo ya kwanza ya kilomita 20 kutoka Kimara-Kivukoni, Kimara-Gerezani na mchepuko wa Morocco.

Kwa kadri miaka inavyosonga, badala ya mradi kuimarika kwa mabasi kuongezeka, unadidimia huku ukiwa hauna changamoto ya kukosa wateja kwa sababu ni wengi kupitiliza.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamilla, hivi karibuni aliishangaa UDART kwa kuendesha mradi wa mabasi kwa takribani miaka mitano pasipo kununua basi jipya hata la dawa tangu kuanza mradi miaka 10 sasa.

Wakati fulani, Mkurugenzi Mkuu wa UDART, Waziri Kindamba, kupitia ujumbe uliowekwa kwenye ukurasa wa TAMISEMI, alisema mabasi mapya 100 yangeingizwa katika mradi huo.

"Kwa hiyo Aprili 2025, tutapokea gari la kwanza la majaribio, lakini ni matumaini yetu pia kwamba yale mengine 99 sasa yatafika kabla ya mwaka wa serikali 2024/2025 kupinduka," alisema Kindamba, na kuongeza kwamba mabasi hayo yanatengenezwa China.

"Swali linaweza kuja kutoka kwa Mtanzania kwa nini yamechoka katika miaka tisa hadi kumi, ukweli ni kwamba magari haya yanafanya kazi siku saba za wiki, masaa takribani 24 kwa sababu yanaanza saa 10 alfajiri mpaka saa sita za usiku," alifafanua Kindamba.

Kwa hiyo ni magari ambayo yapo kwenye kazi wakati wote 'day in day out', kwa hiyo inawezekana kabisa yapo baadhi ya magari machache yakawa na mapungufu ya hapa na pale, ndiyo maana kama menejimenti mpya tumeamua kufanya maamuzi ya kuleta magari mapya yanayotumia teknolojia ya gesi iliyosindikwa".

Hayo ndiyo yalikuwa maneno ya Kindamba, sasa yalifika au hayakufika, huenda hiyo ni stori nyingine ila hali si hali na abiria wa mabasi hayo ni mashahidi wa jinsi wanavyoteseka.

Wakati usafiri huo wa awamu ya Kwanza ukiwa hivyo, serikali imeendelea kujenga barabara za mabasi hayo jijini Dar es Salaam kwa kiwango cha kustahili pongezi.

Dhamira ya serikali ni kuona usafiri katika majiji, likiwemo la Dar es Salaam unakuwa wa uhakika na ustaarabu, ndiyo maana inawekeza mabilioni ya fedha kujenga miundombinu ya mabasi yaendayo haraka.

Miundombinu ya mabasi ya mwendokasi imeendelea kujengwa katika barabara za Kilwa kwenda Mbagala, Barabara ya Nyerere kwenda Gongolamboto, pia katika barabara ya Ali Hassan Mwinyi.

Mapema ilielezwa mradi unatekelezwa kwa awamu sita, ukihusisha mtandao wa njia za mabasi hayo wenye urefu wa kilomita 154.4, ambapo awamu ya kwanza ni kilomita 20.9 zilizokamilika mwaka 2015, na utoaji huduma kuanza Mei 2016, chini ya UDART ambaye ilielezwa ni mtoa huduma wa mpito.

Kwa awamu ya pili ni njia katika barabara ya Kilwa, ambayo nayo imekamilika, huku ujenzi ukiendelea katika barabara zingine.

### MTOA HUDUMA WA MPITO

"Kwa sasa hivi tunamtoa huduma wa mpito ambayo ni kampuni ya UDART," aliwahi kusema Dk. Kihamia na kuongeza kwamba "anatafutwa mtoa huduma kamili na kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha DART, mtoa huduma atatakiwa kuwa ni mtoa huduma binafsi yaani 'private company'.

Alisema mchakato wa kupata mtoa huduma binafsi ulianza tangu wakati wa uongozi wa nchi wa Rais Dk. John Magufuli, na kampuni zaidi ya 30 ziliomba kutoa huduma.

"Katika mchakato huo mchujo uliendelea zikafaulu kampuni saba, miongoni mwao kwa waliofanikiwa katika kampuni hizo saba ni Emirate National Group yenye makao yake makuu Falme za Kiarabu, wakala wakaanza majadiliano na ENG kwa bahati mbaya katika majadiliano ilishindikana kukubaliana kwenye kipengele cha bei", alifafana Dk. Kihamia.

Alisema 2020 mwanzoni zabuni ilitangazwa upya kampuni 40 zilizoomba zikiwemo zile za 2017, mchujo ukafanyika kwa mujibu wa sheria na ENG kupita.

Kabla ya kusaini mkataba, ENG ikatoa hoja kuwepo kipengele cha msuluhishi wa kimataifa ikiwa utajitokeza mvutano katika utoaji wa huduma, kwa sababu mkataba ni wa miaka 12 na chochote kinaweza kutokea.

Pia kulikuwa na kipengele kwamba wakati wowote mtoa huduma akionekana anasuasua au kwa namna yoyote ile mambo yake hayaendi sawa, mkataba utavunjwa mara moja.

"Hilo nalo likawa ni mambo ya kujadiliana ambayo hawakuyakubali, kwa hiyo serikali nayo ikawa inaboresha sheria, yakaweza kufanikiwa," alisema Dk. Kihamia.

Alisema mwaka juzi yalifanyika mabadiliko ambapo msuluhishi wa kimataifa alikubalika na kipengele cha mkataba kuvunjwa kwa sababu za changamoto ndogondogo kikaondolewa.

Kwa hatua hiyo, ni kwamba siku si nyingi usafiri wa awamu ya kwanza ya mradi wa mabasi yaendayo haraka utaimarika na kuwa mzuri huenda zaidi ya ulivyokuwa katika miezi ya mwanzoni ulipozinduliwa.

Hadi kufika Oktoba, Dk. Kihamia amesema mabasi ya mwendokasi 932 yatakuwa yamewasili nchini na kumaliza kero ya abiria kukaa muda mrefu vituoni na mabasi kujaza abiria kupita kiasi, hapana shaka hii ni ahadi kamilifu.

"Mabasi 972 yatakuwa yameondoa kabisa tatizo la msongamano, tatizo la wananchi kuchelewa kufika kituo kimoja hadi kingine, tatizo la kusubiri kwa muda mrefu katika kituo kimoja, kwa bahati nzuri sasa hivi nauli kwenye mabasi haya zitakusanywa kwa kutumia kadi DART APP, ambayo kwenye simu unaweza ukanunua tiketi kama vile SGR," alifafanua.

Alisema awamu ya kwanza ya mradi utakuwa na watoa huduma wawili, awamu ya pili watoa huduma watatu, awamu ya tatu ya mradi utakuwa na watoa huduma kati ya wawili mpaka watatu, awamu ya nne ya mradi itakuwa na watoa huduma wawili.

"Kwa hiyo ukiangalia vizuri ni kwamba awamu zote nne zitakuwa na watoa huduma wasiopungua wanane," alisema Dk. Kihamia.

### KUTELEZA SI KUANGUKA

Kwa kuwa nia ya serikali ni kuona jiji la Dar es Salaam linakuwa la kisasa kwa uwepo wa usafiri wa kisasa, na kwa kuwa awamu ya kwanza ya mradi haikufanya vizuri kama ilivyotarajiwa, wahenga walisema kuteleza si kuanguka.

DART chini ya uongozi wa Dk. Kilamia, hapana shaka itasimama imara kuhahikisha usasa huo katika jiji la Dar es Salaam unakuwa si ndoto bali hali halisi kwa masilahi ya abiria.

Itoshe kusema 'mtoa huduma wa mpito' amedhihirisha alikuwa wa mpito, hata abiria wameonja na wanaendelea kuonja joto ya jiwe kutoka kwake, amekuwa darasa!



CamScanner